
NISHATI
HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati.go.tz Wizara ya Nishati wizara_ya_nishati_tanzania @Nishati2017 Wizara ya Nishati
Toleo Namba 29
Agosti 1 - 31, 2021

# VIONGOZI WAKUU WASTAAFU WATEMBELEA MRADI WA JULIUS NYERERE

## >> MRADI WAFIKIA ASILIMIA 54.3




*Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya kumaliza kukagua mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*



*Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya kumaliza kukagua mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*



*Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. John Malecela akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya kumaliza kukagua mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**

# VIONGOZI WAKUU WASTAAFU WATEMBELEA MRADI WA JULIUS NYERERE

**Hafsa Omar- Rufiji**

Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wastaafu, Waheshimiwa Marais na Mawaziri Wakuu wametembelea mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP) katika Mto Rufiji kwa lengo la kujionea maendeleo ya mradi.

Viongozi hao walitembelea mradi huo, Julai 5, 2021 ambapo katika ziara hiyo waliambatana na Mawaziri mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na Viongozi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Wakizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza kukagua mradi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mhe. Ali Hassan Mwinyi alisema amefurahishwa na namna wataalamu wa kitanzania walivyoweza kusimamia mradi huo kwa ustadi mkubwa hivyo aliwapongeza kwa kutumia vyema taaluma yao kusimamia ujenzi wa mradi huo.

Kwa upande wake,



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumaliza kukagua mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*




*Picha ya Pamoja ya Viongozi Wakuu Wastaafu wakiwa na viongozi wa Wizara ya Nishati.*

# VIONGOZI WAKUU WASTAAFU WATEMBELEA MRADI WA JULIUS NYERERE

INATOKA UK.2

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alimpongeza Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa ujasiri wa kuamua mradi ujengwe na kwa kutumia fedha za ndani ili kutimiza ndoto ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Alieleza kuwa, ndoto ya Baba wa Taifa ilikuwa ni kujenga bwawa kubwa la kuzalisha umeme, lenye shughuli ya utalii, litakalopunguza mafuriko sehemu ya chini ya mto Rufiji na kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kitakacholisha takribani watu milioni 20, na kuwataka wadau wa kilimo kuanza kujipanga kutumia fursa ya kilimo cha umwagiliaji.

Naye, Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. John Malecela, alisema kuwa tangu taifa lipate uhuru halijawahi kutekeleza mradi mkubwa kama huo wa kufua umeme kwa maji na kuwataka Watanzania kulinda mradi huo.

Mhe. Malecela, alisema watanzania wanapaswa kujivunia na kujisikia fahari kwani mradi huo unasimamiwa na wazawa ambao wameonesha uzalendo kwa taifa kwa kusimamia vyema ujenzi wake.

Waziri Mkuu Mstaafu, Cleopa









*Picha za matukio mbalimbali wakati wa ziara ya Viongozi Wakuu Wastaafu katika mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*

# VIONGOZI WAKUU WASTAAFU WATEMBELEA MRADI WA JULIUS NYERERE

Msuya alimpongeza Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na wataalamu wa Wizara ya Nishati kwa kujitoa na kuwajibika kikamilifu katika usimamizi wa ujenzi wa mradi huo.

Naye,Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda, aliwataka watanzania kutumia mradi huo vizuri kwasababu utakuwa na fursa nyingi sana ambazo zitawakomboa watanzania kiuchumi.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alieleza kuwa hadi sasa mradi umefikia asilimia 54.3 ambapo kazi kubwa za msingi zimeshafanyika na asilimia zilizobaki zitakamilika ndani ya miezi michache.

Alieleza kuwa,tayari mkandarasi ameshalipwa zaidi ya trilioni mbili na sasa Serikali inaendelea na maandalizi ya kuwalipa tena wakandarasi kwa hatua ya ujenzi waliofikia.

Aidha, alisema mradi ukikamilika nchi itakuwa na umeme wa kutosha, wa uhakika na wenye gharama nafuu hivyo ametoa wito kwa wenye nia ya kuwekeza kujitokeza na kuwekeza kwenye shughuli za kilimo, umwagiliaji na utalii.

Vilevile, alieleza kuwa kupitia uzoefu wa usimamizi wa mradi huo watanzania tumejifunza kwamba hata miradi mingine itakayoanza kutekelezwa itasimamiwa na watanzania wenyewe kwani wataalamu wazawa wanao uwezo huo.







*Picha za matukio mbalimbali wakati wa ziara ya Viongozi Wakuu Wastaafu katika mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere(JNHPP), Julai 5,2021.*

# Makatibu Wakuu waridhishwa na JNHPP, ujenzi wafikia 54%

**Zuena Msuya, Pwani**

Kamati ya Uongozi ya Mradi wa Julius Nyerere inayoundwa na Makatibu Wakuu wa Wizara 15, imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali aliongoza kamati hiyo, Julai 13, 2021, wakati wa ziara ya makatibu wakuu hao ya kutembelea na kukagua mradi huo wa kufua umeme wa Megawati 2,115 kwa kutumia maporomoko ya Maji ya Mto Rufiji, mkoani Pwani.



*Kamati ya Uongozi ya mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) inayoundwa na Makatibu Wakuu wa Wizara 15, wakiwa katika picha ya pamoja baada kufanya ziara ya kukagua mradi huo, Julai 13, 2021.*

Akizungumza kwa niaba ya Makatibu wakuu hao, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Marry Maganga alisema kuwa wamefarijika kuona kasi ya utekelezaji wa mradi huo ambao umefikia asilimia 54 ya ujenzi wa maeneo muhimu ya mradi.

Maganga alisema kuwa Makatibu wakuu wote wanaohusika moja kwa moja na mradi huo, wanaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana kuhakikisha kila kitu kinatekelezeka kwa wakati bila kikwazo chochote ili kuhakika kuwa mradi huo utakamilika kama ulivyopangwa Mwezi Juni 2022.

"Mradi huu unatekelezwa kwa fedha zetu wenyewe watanzania,sisi makatibu wakuu tunajukumu la kuusimamia ipasavyo katika utekelezaji wake kwa kuhakikisha kuwa kila kitu kinaenda



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) akiwa na Kamati ya Uongozi ya Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP), wakipata maelezo ya mradi kutoka kwa Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Mhandisi John Mgeni,(pili kulia) walipofanya ziara ya kukagua mradi huo, Julai 13,2021.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa pili kushoto) akisikiliza jambo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO) Dkt. Tito Mwinuka, (wa pili kulia), wengine ni Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Edward Ishengoma (kushoto) na Naibu Mkurugenzi Mtendaji Uwekezaji wa TANESCO, Mhandisi Khalid James ( kulia) wakati wa ziara ya Kamati ya uongozi ya mradi wa Julius Nyerere(JNHPP), Julai 13,2021.*

# Makatibu Wakuu waridhishwa na JNHPP, ujenzi wafikia 54%

kama inavyotakiwa kurahisisha utekelezaji wa mradi huo, kwa umoja wetu tunajivunia kuwa sehemu ya kutekeleza mradi huu", alisema Maganga.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, aliwaeleza makatibu wakuu hao kuwa, kwa kuwa Wizara ya Nishati ndiyo msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mradi huo itahakikisha inakuwa bega kwa bega na wizara jumuishi kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Aidha Mahimbali alisema kuwa



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akizungumza na Kamati ya uongozi ya mradi wa Julius Nyerere(JNHPP),(hawapo pichani) walipofanya ziara ya kukagua mradi huo, Julai 13,2021.*

wataendelea kumsimamia ipasavyo mkandarasi aliyepewa dhamana ujenzi wa mradi huo ili atekeleze majukumu yake ipasavyo kama ilivyoelekezwa katika makubaliano ya mkataba wa utekelezaji.

"Utekelezaji wa JNHPP uko katika hatua nzuri ya ujenzi katika maeneo yote makuu, ikiwamo Kingo za Bwawa husika, Tuta kuu la Bwawa, Kituo cha Kuchochea Umeme pamoja na Nyumba ya kuendeshea Mitambo ya kuzalisha umeme, mwezi Novemba mwaka huu tutaanza kujaza maji kwa ajili ya kuzalisha umeme kuanzia mwezi juni 2022," alisema Mahimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka aliwataka watanzania kuvuta subira na kuwa na imani na Serikali yao kwakuwa mradi huo



*Viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati, wakifuatilia maelezo ya utekelezaji wa mradi wa Julius Nyerere( JNHPP), kutoka kulia ni Mhandisi Salum Inegeja, Mkurugenzi wa Manunuzi Sharif Fadhili, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Ziana Mlau na Mhasibu Mkuu Michael Marandu, wakati wa ziara ya Kamati ya uongozi ya mradi wa Julius Nyerere(JNHPP), Julai 13,2021.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO) Dkt. Tito Mwinuka, (kulia) akitoa maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Julius Nyerere(JNHPP),kwa Kamati ya uongozi ya mradi huo walipofanya ziara, Julai 13,2021.*

# Makatibu Wakuu waridhishwa na JNHPP, ujenzi wafikia 54%

unatekelezeka na utazalisha umeme kama ilivyokusudiwa.

Aliwaeleza watanzania kuwa mradi huo utakapokamilika utawezesha umeme kuwa mwingi, wa uhakika na kwa gharama nafuu, vilevile hata kuuza nje ya nchi kwa watakaohitaji.

Kamati hiyo ilitembelea na kukagua maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Mradi huo ambayo ni Handaki la Kuchepusha Maji ya Mto, Kingo za Bwawa husika, Tuta kuu la Bwawa, Kituo cha Kuchochea Umeme pamoja na Nyumba ya kuendeshea Mitambo ya kuzalisha umeme.

Aidha walitembelea na kukagua Daraja la Kudumu, Barabara, Njia ya kupitisha maji ya kuzalisha umeme, pamoja na eneo la ufungaji wa mitambo.



*Kamati ya Uongozi ya Mradi wa Julius Nyerere(JNHPP), wakitazama eneo linalojengwa nyumba ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme walipofanya ziara ya kukagua mradi huo, Julai 13,2021.*



*Sehemu ya ujenzi wa daraja la kudumu ukiendelea, daraja hilo litakuwa la pili kwa ukubwa katika Mto Rufiji likitanguliwa na lile la Mkapa.*



*Ujenzi ukiendelea katika Mahandaki Tisa ya kupekeleka maji katika mitambo ya kuzalisha umeme katika mradi wa Julius Nyerere (JNHPP).*

# RAIS SAMIA KUVUNJA REKODI AFRIKA UMEME VIJIJINI



*Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, Mkoa wa Mara, uliofanyika katika kijiji cha Kitunguruma, Kata ya Mbaribari, wilayani Serengeti, Julai 8 mwaka huu.*

**Veronica Simba na Hafsa Omar - Mara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuvunja rekodi kwa Marais wote wa Afrika katika uunganishaji umeme vijijini.

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amebainisha hayo wakati akizungumza na wananchi katika hafla ya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, iliyofanyika katika kijiji cha Kitunguruma, Kata ya Mbaribari, wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara, Julai 8 mwaka huu.

Akifafanua, Dkt. Kalemani alieleza kuwa Tanzania inatarajiwa kuandika historia ya kuunganisha umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo Disemba 2022 hivyo kuongoza katika Bara la Afrika kufikia mafanikio hayo.

"Tulianza utekelezaji wa miradi hii katika ngazi ya wilaya, kisha vijiji ambapo hadi sasa zaidi ya vijiji 10,312 vimeshapelekewa umeme; na vilivyobakia takribani vijiji 1,956 ndivyo vinapelekewa katika mradi huu," alibainisha Waziri.

Akieleza zaidi, Dkt Kalemani alisema mafanikio hayo makubwa yametokana na uongozi mzuri wa Rais Samia ambaye Serikali anayoiongoza imedhamiria kwa dhati kuleta maendeleo kwa wananchi.

Awali, akielezea utekelezwaji wa Mradi huo katika Mkoa wa Mara, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi



*Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, akipunga mikono kuwasalimu wananchi wa kijiji cha Gibaso, Kata ya Kwihancha, wilayani Tarime, Mkoa wa Mara, ambapo Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) alisimama kuzungumza nao baada ya kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, uliofanyika katika kijiji cha Kitunguruma wilayani Serengeti, Julai 8, 2021.*

# RAIS SAMIA KUVUNJA REKODI AFRIKA UMEME VIJIJINI



*Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Gibaso, Kata ya Kwihancha, wilayani Tarime, Mkoa wa Mara, baada ya kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, uliofanyika katika kijiji cha Kitunguruma wilayani Serengeti, Julai 8, 2021.*

Amos Maganga, alibainisha kuwa utagharimu takribani shilingi bilioni 9.63

Aidha, aliongeza kuwa Mradi umelenga kuvifikishia umeme vijiji 45 vya Mkoa huo ambavyo ndivyo pekee vilivyosalia kati ya vijiji vyake vyote 459.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mbunge wa Serengeti Amsabi Mrimi na Mbunge wa Tarime Vijijini Mwita Waitara, waliipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya usambazaji umeme vijijini na kuahidi kuwa wananchi wao wako tayari kupokea umeme na kuutumia kwa shughuli za maendeleo.

Hafla hiyo ya uzinduzi ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama vya siasa na wananchi.



*Wananchi wa Kijiji cha Kitunguruma, Kata ya Mbaribari, wilayani Serengeti, Mkoa wa Mara, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, uliofanyika katika kijiji hicho, Julai 8, 2021.*



*Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akiwatambulisha wakandarasi, Kampuni ya Gizal Cable Industries Ltd, watakaotekeleza Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza, Mkoa wa Mara. Waziri alizindua rasmi Mradi huo Ngazi ya Mkoa katika kijiji cha Kitunguruma wilayani Serengeti, Julai 8, 2021.*



*Wananchi wa Kijiji cha Gibaso, Kata ya Kwihancha, wilayani Tarime, Mkoa wa Mara, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) aliyesimama kuzungumza nao baada ya kuzindua rasmi Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, katika hafla iliyofanyika katika kijiji cha Kitunguruma, Kata ya Mbaribari, wilayani Serengeti, Julai 8, 2021.*

# NAIBU WAZIRI BYABATO AZINDUA MRADI WA REA III MZUNGUKO WA PILI TANGANYIKA



*Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Wakili Stephen Byabato akizungumza na wanakijiji cha Ilangu wakati wa uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Ilangu, kata ya Ilangu, tarafa ya Kabungu, wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi tarehe 13 Julai 2021.*

**Na Dorina G. Makaya - Katavi**

Naibu Waziri wa Nishati , Wakili Stephen Byabato amefanya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Ilangu, kata ya Ilangu, tarafa ya Kabungu, wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi.

Akizungumza tarehe 13 Julai, 2021,wakati wa hafla ya uzinduzi, Naibu Waziri Byabato alisema, zaidi ya shilingi bilioni 15 zitatumika kuvipelekea umeme vijiji 25 vya wilaya ya Tanganyika.

Alisema, kwa kijiji cha Ilangu peke yake, takriban shilingi milioni 618 zitatumika kuunganisha umeme.

Alisema, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji umeme nchi nzima na kuwa upatikanaji wa umeme vijijini utachangia kuongezeka kwa kasi ya uanzishwaji wa viwanda vya uchakataji wa mazao na kuwa kichocheo cha ukuaji wa biashara na uchumi kiujumla.

Naibu Waziri Byabato aliwaambia wanakijiji cha Ilangu kuwa, Serikali imewapunguzia wananchi gharama ya kuunganishiwa umeme kutoka shilingi 177,000 hadi shilingi 27,000 tu kwa wateja wa umeme wa njia moja na kwa wateja wa umeme wa njia tatu kutoka shilingi 912,000 hadi shilingi 139,500 ili kuwawezesha wananchi kuunganishiwa umeme.

Alisema, kwa mwananchi ambaye atakuwa hajakamilisha kupata pesa kamili za kulipia anaweza kulipa kidogo kidogo ndani ya kipindi cha Mradi wa eneo husika na atakapokamilisha ataunganishiwa umeme.

Naibu Waziri Byabato alimtaka mkandarasi wa Mradi kuhakikisha anawaunganishia umeme wateja wote bila kujali aina ya nyumba anayoishi na kutoa kipaumbele kwa taasisi na maeneo yanayotoa huduma za kijamii kama vile vituo vya afya, shule, nyumba za ibada, ofisi za Serikali, visima vya maji pamoja na viwanda vidogo ambavyo vitachangia kasi ya maendeleo katika eneo husika na Taifa kiujumla.

Alieleza kuwa, kupatikana kwa umeme katika kata ya Ilangu pamoja na maeneo mengine ya



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Wakili Stephen Byabato (wa pili kulia) akizindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Ilangu, kata ya Ilangu, tarafa ya Kabungu, wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi tarehe 13 Julai 2021.*

# NAIBU WAZIRI BYABATO AZINDUA MRADI WA REA III MZUNGUKO WA PILI TANGANYIKA



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Wakili Stephen Byabato (wa pili kulia) akimtambulisha mkandarasi wa ujenzi wa umeme kwa wanakijiji cha Ilangu wakati wa Uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Ilangu, kata ya Ilangu, tarafa ya Kabungu, wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi tarehe 13 Julai 2021.*

vijiji ambavyo bado havijaunganishiwa umeme, kutachochea ukuaji wa viwanda vikiwemo vya kuchakata mazao, vya kusaga na vya uchomeleaji.

Naibu Waziri Byabato alisema, ili kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda kulipia gharama za kuunganishiwa umeme, Serikali imemuelekeza Mkandarasi kufungua ofisi katika eneo linalotekelezwa mradi na kuwa hakuna mwananchi anayetakiwa kulipia nguzo.

Aliwaasa wananchi kutunza miundo mbinu ya umeme na kubainisha kuwa, Mradi wa REA hauna fidia.

Aliwaomba wananchi wa eneo la mradi kutoa ushirikiano katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi na kuwataka kutumia fursa hiyo kujipatia ajira za muda.

Aliwaasa wanakijiji hao, kuepuka tabia ya kuharibu miundo mbinu ya umeme ili kuhakikisha umeme unaendelea kupatikana.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Rojers Romuli, aliishukuru Serikali kwa uamuzi wa kuvipelekea umeme vijiji vya Halmashauri ya Tanganyika na kusema kuwa, hatua hiyo itachangia katika kuongezeka kwa kasi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

Naye mbunge wa Jimbo la Tanganyika Mkoa wa Katavi Mhe. Moshi Kakoso aliwataka wanakijiji cha Ilangu na wananchi wote wa jimbo la Tanganyika kuitumia vema fursa ya umeme jimboni humo ili kujiletea maendeleo.

Jumla ya shilingi bilioni 24.7 zitatumika kuviunganishia umeme vijiji 53 ambavyo bado vilikuwa havijapata umeme katika mkoa wa Katavi



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Wakili Stephen Byabato akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, baadhi ya watumishi wa Wizara ya Nishati, TANESCO na REA mara baada ya uzinduzi wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili katika kijiji cha Ilangu, kata ya Ilangu, tarafa ya Kabungu, wilaya ya Tanganyika, mkoa wa Katavi tarehe 13 Julai 2021.*

# Nishati inaakisi Kauli Mbiu ya Maonesho ya Sabasaba- Mahimbali




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah wakipata maelezo mara baada ya kutembelea Banda la Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

**Teresia Mhagama na Zuena Msuya, DSM**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali amesema sekta ya nishati inaakisi kauli mbiu ya Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ambayo ni Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu.

Mahimbali alisema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea baadhi ya mabanda ya washiriki wa Maonesho hayo katika viwanja vya Mwalimu Nyerere, mkoani Dar es Salaam, Julai 4, 2021, ambapo aliambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah

Alifafanua kuwa nishati inaakisi kauli mbiu ya Maonyesho hayo kwa kuwa vitu vyote vilivyolengwa katika kauli mbiu hiyo vinategemea zaidi uwepo wa nishati ya uhakika katika




*Mhandisi Mitambo kutoka Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Amani Christopher akiwaonesha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah modeli ya Mtambo wa Matumizi ya Jotoardhi katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

# Nishati inaakisi Kauli Mbiu ya Maonesho ya Sabasaba- Mahimbali



*Kaimu Meneja Miradi, Mipango na Utafiti kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Jensen Mahavile akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah masuala ya umeme vijijini mara baada ya kutembelea banda la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

utekelezaji wake.

"Nimefarijika sana kutembelea maonesho haya ya Sabasaba, nimewasikiliza wafanyabiashara kila mmoja kwa nafasi yake amekuwa akizungumzia nishati ya Umeme kwa namna ambavyo anaitumia kuboresha Biashara yake kwa namna moja ama nyingine kwa maeneo ya vijijini ni Mijini", alisema Mahimbali

Aliongeza kuwa, inadhihirisha wazi kuwa



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah wakiangalia majiko yanayotumia teknolojia ya sumaku katika Banda la Wakala wa Nishati Vijijini katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

# Nishati inaakisi Kauli Mbiu ya Maonesho ya Sabasaba- Mahimbali

nishati ya Umeme ni mkombozi mkubwa wa ukuaji wa uchumi wa nchi na mwananchi mmoja mmoja.

Aidha aliwaasa watanzania kujitokeza kwa wingi kutembelea Banda la Nishati pamoja na Taasisi zake, ili kuona, kujifunza na kupata uelewa zaidi juu ya shughuli zinazofanywa na wizara pamoja na Taasisi zake.

Vilevile aliwaeleza watanzania kuwa wafike katika mabanda hayo ili kuona mfano wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji, pamoja na kupata maelezo ya namna mradi huo unavyotekelezwa na hatua iliyofikiwa hadi sasa katika ujenzi wake.

Aliongeza kuwa katika maonesho hayo,



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah wakiangalia mita za umeme zinazozalishwa hapa nchini katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*



*Mhandisi Mradi kutoka mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah kuhusu mradi huo katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

# Nishati inaakisi Kauli Mbiu ya Maonesho ya Sabasaba- Mahimbali




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kushoto) akimkabidhi Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah vitabu vya Sera ya Nishati pamoja Mpango Kabambe wa Umeme mara baada ya kutembelea banda la Wizara ya Nishati katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

alitembelea mabanda mbalimbali ikiwepo la Wizara ya Nishati na taasisi zilizochini yake ambazo ni Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Kampuni ya Uendelezaji Joto Ardhi ( TGDC), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja( PBPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Mamlaka ua Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

watanzania wameona namna ambavyo Joto Ardhi linavyozalisha umeme kwa kutumia mvuke unaotoka chini ya ardhi.

Pia, aliwakumbusha watanzania kutumia nishati ya Umeme katika kujiletea maendeleo kwa kuwa serikali inatumia nguvu kubwa kuhakikisha kuwa nishati hiyo inasambazwa nchi nzima kwa gharama nafuu.

Akiwa katika viwanja hivyo vya Mwalimu Nyerere, Mahimbali




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, akisaini kitabu cha wageni baada kutembelea Banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli( PURA) katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Julai 4,2021.*

# WATANZANIA WATAKIWA KUTUMIA FURSA ZA UJENZI BOMBA LA MAFUTA

**Hafsa Omar-Kagera**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amewataka wananchi watakaopitiwa na ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kujitokeza na kuzitumia fursa mbalimbali ambazo zitapatikana wakati wa ujenzi wa bomba hilo.

Aliyasema hayo, Julai 17, 2021 wakati wa mkutano na wadau mbalimbali kujadili fursa za Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta, uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, mkoani Kagera.

Dkt. Kalemani alizitaja baadhi ya fursa hizo kuwa ni ujenzi wa viwanda mbalimbali vitakavyozalisha bidhaa ambazo zitatumika katika ujenzi wa mradi.

Pia, alisema Watanzania zaidi ya 15,000 wataajiriwa katika kipindi cha ujenzi wa bomba hilo na kuwataka kuchangamkia fursa ya kufanya biashara mbalimbali ambazo zitawaingizia kipato.

Alisema, lengo la mkutano huo ni kujenga uelewa na kuwaeleza wananchi wajibu wao ili waweze kushiriki katika shughuli mbalimbali wakati wa ujenzi husika, ambapo ameeleza kuwa zaidi ya asilimia 80 ya kazi za mradi huo zitafanywa na Watanzania.

"Mradi huo wakati



Mkuu wa Mkoa wa Kagera Meja Jenerali Charles Mbuge akizungumza katika wa Mkutano na wadau kujadili fursa za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera Julai 17,2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza katika wa Mkutano na wadau kujadili fursa za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera Julai 17,2021.



Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Petro Marwa (kushoto) Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt. James Mataragio(katikati) wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(hayupo pichani) wakati wa Mkutano na wadau kujadili fursa za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera Julai 17,2021.

# WATANZANIA WATAKIWA KUTUMIA FURSA ZA UJENZI BOMBA LA MAFUTA





*Washiriki wakisikiliza mada mbalimbali zilizotolewa katika Mkutano wa wadau kujadili fursa za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera Julai 17,2021.*

wa ujenzi utatoa fursa kwa Watanzania wengi, tunawaomba Watanzania kuchukua nafasi hii kuwekeza katika sekta mbalimbali, na kwa wale ambao hawana mtaji tunaongea na mabenki ili waweze kuwakopesha mikopo ya masharti nafuu."alisema

Aidha, alisema utekelezaji wa mradi umeanza na upo kwenye hatua za mwisho za ulipaji wa fidia na baadhi ya maeneo tayari ujenzi wa barabara za kuelekea kwenye mradi umeanza.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa mradi huo utachukua takribani miaka mitatu na utagharimu dola za kimarekani bilioni 3.5

Waziri Kalemani, pia alieleza manufaa ya mradi huo kwa kufafanua kuwa katika Mikoa ya Singida, Tabora na Simiyu, maeneo hayo ambayo bomba linapita yanatarajiwa nayo kutoa mafuta ambapo alisema nchi itatumia bomba hilo kupitisha mafuta hayo.

Pia, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali pamoja na

# WATANZANIA WATAKIWA KUTUMIA FURSA ZA UJENZI BOMBA LA MAFUTA

wawekezaji na kushiriki katika ulinzi wa bomba hilo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kagera Meja Jenerali Charles Mbuge alisema, ujenzi wa mradi huo utainua uchumi wa Mkoa wa Kagera na kwa nchi kiujumla.

Vilevile, alisema atahakikisha mradi utajengwa na kusimamiwa kwa umakini, na mataifa mengine yatajua kuwa Watanzania ni watu makini na wazalendo na hilo litasadia nchi kuendelea kupata fursa mbalimbali za miradi kutoka kwenye mataifa ya jirani.

Pia, alisema kuwa uongozi wa Mkoa huo utahakikisha mradi huo unalindwa na utakuwa kuwa salama mda wote wa ujenzi na hata ukikamilika.

Naye, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kuchukua fursa mbalimbali ambazo zitapatikana kwenye ujenzi wa mradi na kuwataka kujivunia ujenzi huo kwani unaenda kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali Mkoa wa Kagera na Wizara mara baada kumaliza kwa Mkutano wa wadau kujadili fursa za mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), uliofanyika katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera, Julai 17, 2021*

# Kituo cha kupoza Umeme kujengwa Kongwa

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema Serikali itajenga kituo kikubwa cha kupoza Umeme katika Wilaya ya Kongwa ili kumaliza tatizo la kukatika umeme mara kwa mara na kuboresha upatikanaji wa umeme katika wilaya hiyo na maeneo jirani.

Dkt. Kalemani alisema hayo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na kutembelea eneo litakalojengwa kituo hicho lililopo katika Kijiji cha Machenje Kata ya Ugogoni Wilayani ya Kongwa mkoani Dodoma,Julai 27,2021.

Katika ziara hiyo, Dkt. Kalemani alisema kuwa tayari eneo la ukubwa wa Hekari 130 limepatikana ambalo litatumika kujenga kituo hicho, kitakachokuwa na uwezo wa kufua umeme wa Kilovoti 220.

Aidha alisema kuwa tayari zaidi ya shilingi milioni 63 zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wakazi wa eneo hilo watakaopisha ujenzi wa mradi husika ambao utagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 41.2.

Ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kuanza kutekelezwa mapema mwezi Septemba mwaka huu 2021.

"Tuna umeme mwingi sana Mkoa wa Dodoma, lakini kuna changamoto kubwa ya kukatika umeme na wenye nguvu ndogo katika maeneo yote ya Wilaya ya Kongwa, hii inatokana na umeme huo kusafiri umbali mrefu kutoka kituo cha




*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(kulia) akizungumza na wakazi wa Kibaigwa wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya umeme katika Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Julai 27, 2021.*

# Kituo cha kupoza Umeme kujengwa Kongwa



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Antony Mtaka (kushoto) na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai( kulia) akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Machenje kitakapojengwa kituo cha kufua umeme cha Kongwa, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati ya kukagua miundombinu ya umeme katika wilaya hiyo, mkoani Dodoma, Julai 27, 2021.*

Zuzu hadi kufika huku takribani kilomita 120 na mzunguko ni takribani Kilomita 2000, suluhisho la kudumu ni ujenzi wa kituo cha kufua umeme ambacho kitamaliza kabisa tatizo hilo na kuwa historia, hasa katika Viwanda, Wafanyabiashsa na watumiaji wengine", alisema Dkt. Kalemani

Hata hivyo alisema kuwa, katika kutatua tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika maeneo ya Mbande, Kibaigwa, Kongwa, Mpwapwa na Kiteto, ndani ya wiki hii kitafungwa kifaa maalum, kinachojulikana kama AVR ili kuuongeza nguvu ya Umeme katika maeneo hayo.

Dkt. Kalemani alifafanua kuwa kifaa hicho tayari kimeshatoka mkoani Ruvuma kuja Dodoma na kufungwa katika eneo la Mbande.

Sambamba na hilo kazi ya Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme wa kV 220 inaendelea kujengwa kutoka Zuzu kupitia Mpunguzi hadi kufika wilayani humo ili kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo tajwa na mengine jirani.

Ujenzi wa njia hiyo ya umeme umefikia zaidi ya 55%.

Kufuatia utekelezaji wa miradi hiyo, aliwataka wakazi wa maeneo hayo kuvuta subira wakati tatizo la kukatika Umeme na kusambaza Umeme katika maeneo ambayo hayakufikiwa likitatuliwa hivi karibu.

Aidha aliweka wazi

# Kituo cha kupoza Umeme kujengwa Kongwa

kuwa kuanzia mwaka wa fedha ujao, mkoa wa Dodoma utagawanywa Kitanesco na kuwa kama majiji mengine ikiwemo Dar es Salaam kwa lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za umeme kwa wateja.

Vilevile alitumia ziara hiyo kukipandisha hadhi kituo cha umeme cha Kibaigwa kuwa kituo cha Wilaya ili kuimarisha na kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo.

Akizungumzia suala la usambazaji wa umeme vijijini, Dkt. Kalemani alimtaka mkandarasi kuongeza kasi katika kutekeleza kazi hiyo na kwamba wananchi wote waliolipia waunganishiwe umeme kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka aliwataka wakazi wa eneo litakalojegwa kituo cha kupoza umeme kuwa walinzi wa kituo hicho na kutoa ushirikiano kwa watakaotekeleza kazi hiyo.

Vilevile aliwataka wakazi wa maeneo ambayo bado hayajafikiwa na umeme kujiandaa kuupokea umeme huo kwa kutandaza nyaya katika nyumba zao pamoja na kulipia ili kuwa tayari kuunganishiwa umeme.

Mkoa wa Dodoma una wakandarasi 3 ambao watatekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vyote vilivyosalia kwa kipindi cha miezi 12 na kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Mkoa wa Dodoma kwa sasa unaongoza kwa kuwa na megawati zaidi ya 640 za umeme ukifuatiwa na mkoa wa Dar es Salaam wenye megawati zaidi ya 500.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (pili kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Antony Mtaka (tatu kushoto ) na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai (nne kushoto) pamoja na viongozi wengine wakiwasili katika Kijiji cha Mbande, kutakapofungwa kifaa cha AVR wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya umeme katika wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma, Julai 27, 2021.*

# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 42 KUBORESHA UMEME TABORA – BYABATO



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akizungumza na Waandishi wa Habari alipotembelea kituo cha kupozea na kusambaza umeme cha Kiloleni kilichopo Tabora mjini, mkoani Tabora tarehe 10 Julai, 2021.*

**Na Dorina G. Makaya - Tabora**

Zaidi ya shilingi bilioni 42 zimetengwa na Serikali kwa ajili ya kuboresha kituo cha kupozea na kusambaza umeme cha Kiloleni, wilayani Tabora mjini, mkoani Tabora ili kuimarisha huduma ya umeme mkoani humo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato tarehe 10 Julai, 2021 alipotembelea kituo cha kupozea na kusambaza umeme cha Kiloleni kilichopo Tabora mjini, mkoani Tabora.

Naibu Waziri Byabato alisema, Tabora ni mkoa wa kimkakati wenye fursa nyingi za maendeleo ikiwemo migodi, kilimo na viwanda hivyo, unahitaji kuwa na umeme wa uhakika kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika kwa kasi.

Aliongeza kuwa, umeme wa uhakika mkoani Tabora utawezesha uendeshaji wa treni ya kisasa (Standard Gauge)



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akipata maelezo kutoka kwa msimamizi wa Kituo cha Kiloleni Frank Chengula namna chombo cha kuongozea mitambo kinavyofanya kazi kituoni hapo tarehe 10 Julai, 2021.*

# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 42 KUBORESHA UMEME TABORA – BYABATO



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Mwandamizi wa Mifumo ya Umeme wa Kanda ya Magharibi TANESCO, Yahya Ngasongwa kuhusu upokeaji na usambazaji wa umeme kituoni hapo tarehe 10 Julai, 2021.*

ambayo uzinduzi wa shughuli za ujenzi wake unatarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Naibu Waziri Byabato alieleza kuwa, kituo cha kupozea na kusambaza umeme cha Kiloleni, kinachopokea umeme kutoka mkoa wa Shinyanga na kusambaza katika wilaya za Tabora, Sikonge, Urambo, Kaliua na Uyui kikiwa na megawati 24 kilianza kazi mwaka 1989 hivyo ni muhimu kukiboresha ili kiwe na umeme wa uhakika na kuwa fedha zilizotengwa zitapelekea kituo hicho kuwa na megawati 72.

Aidha, Naibu Waziri Byabato alibainisha kuwa, Kituo cha kupozea na kusambaza umeme cha Kiloleni ni miongoni mwa vituo 9 vinavyotarajiwa kuboreshwa mkoani Tabora ili kuwa na umeme wa uhakika.

Vilevile, Naibu Waziri Byabato aliagiza kutengenezwa kwa transfoma iliyoharibika ndani ya Mwezi Julai, 2021 ili kuongeza nguvu ya umeme kituoni Kiloleni licha ya kuwa kuna transfoma moja inayofanya kazi.

Aidha, Naibu Waziri Byabato alieleza kuridhishwa kwake na utendaji wa Ofisi ya TANESCO Mkoa wa Tabora na kuwataka waendelee kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi ili kufikia malengo ya Kitaifa katika sekta ya Nishati.

# DKT KALEMANI AAGIZA TRANSFOMA ZITOKE BANDARINI

**Hafsa Omar-Dar es Salaam**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, amesema ifikapo tarehe 12 mwezi huu transfoma zote sita ambazo zipo Bandari ya Dar es Salaam ziwe zimeshasafirishwa kwenda kwenye ujenzi wa mradi wa bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere(JNHPP).

Aliyasema hayo, 4 Julai, 2021 wakati wa ziara ya kushtukiza kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, aliambatana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka.

Dkt. Kalemani,alisema



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza kufanya ziara ya kushtukiza katika bandari ya Dar es Saalam, Julai 4,2021.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani,(kushoto) Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali(katikati) wakiwasili katika Bandari ya Dar es Salaam kwaajili ya ziara ya kushtukiza, Julai 4,2021.*

# DKT KALEMANI AAGIZA TRANSFOMA ZITOKE BANDARINI

amefanya ziara hiyo ili kujua sababu ambazo zimepelekea kucheleweshwa kwa kuondolewa kwa Transfoma hizo katika bandari hiyo, ambapo zinatakiwa kupelekwa katika mradi wa Julius Nyerere ili kuendelea na ujenzi wa mradi huo.

Alieleza kuwa, mwezi uliopita alipotembelea mradi wa Julius Nyerere alihakikishiwa kuwa transfoma hizo zitafika kwa wakati katika mradi huo lakini mpaka sasa bado zipo bandarini.

" hizi Transfoma zimekwamishwa na nini , kwanini zimalize mwezi mzima bandarini na wakati zilitakiwa ziwe zimetoka naomba niseme sitavumilia hii hali, huu mradi wenyewe ni wa haraka haraka kila mmoja anauhitaji kwahiyo hatutavumilia mtu yoyote atucheleweshe,"alisema.

Aidha, aliwataka waatalam wote ambao wanahusika na nyaraka ambazo zinahusika na uletaji wa vifaa nchini, wakizipata nyaraka hizo waanze maramoja taratibu zote za utoaji wa mizigo bandarini.

Pia, aliwataka watumishi wa bandari kutoa ushirikiano kwa Wizara ili kuweza kutatua changamoto zozote ambazo zitajitokeza na kuwataka kuwasiliana na viongozi wa Wizara ili kumaliza changamoto hizo kwa haraka.




*Transfoma ikiwa tayari imepakiwa kwenye gari kwaajili ya kupelekwa katika mradi wa bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere(JNHPP).*

"Hatutaki kuona vifaa vinavyokwenda kwenye miradi vinakaa bandarini, mahala pake pa kukaa sio bandarini ni kwenye miradi na Mhe. Rais ametupa fedha tena za kutosha na mkandarasi hadai chochote kwahiyo hivi vifaa vinatakiwa kuwa kwenye mradi ili mkandarasi aendelee na kazi," alisisitiza Dkt. Kalemani



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, watumishi wa bandari,wakiwa katika ziara katika bandari ya Dar es Saalam, Julai 4,2021.*

# Mkandarasi ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mradi wa JNHPP aanza kazi

**Na Teresia Mhagama, DSM**

Imeelezwa kuwa, Mkandarasi atakayejenga njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 kutoka eneo la mradi wa umeme wa Julius Nyerere ( JNHPP), Rufiji mkoani Pwani hadi Chalinze ameanza kazi.

Hayo yalitanabaishwa wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali mkoani Dar es Salaam na Pwani iliyolenga kukagua maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupoza umeme utakaotoka katika Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.

Viongozi hao waliambatana na Makamishna na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali kutoka Wizara hizo mbili pamoja na watendaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka.



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na watendaji kutoka Wizara hizo wakiwa katika eneo la Chalinze mkoani Pwani kutakapojengwa kituo kipya cha kupoza umeme utakaotoka katika Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.*

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO-Uwekezaji, Khalid James alisema kuwa, ujenzi wa njia hiyo ya kusafirisha umeme itakuwa na urefu wa kilometa 160 na kwamba wananchi takriban 300 waliopisha maeneo yatakapojengwa miundombinu hiyo ya usafirishaji umeme wameshalipwa fedha zao na hivyo wamebaki takriban wananchi 100 tu kulipwa fidia.

Alitaja kampuni inayotekeleza mradi huo kuwa ni Larsen & Toubro kutoka India.

Aliongeza kuwa, katika eneo la Chalinze kutajengwa kituo kipya cha kupoza umeme unaotoka katika mradi



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na watendaji kutoka Wizara hizo wakiwa katika eneo la Kinyerezi mkoani Dar es Salaam kutakapojengwa kituo kipya cha kupoza umeme utakaotoka katika Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.*

# Mkandarasi ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mradi wa JNHPP aanza kazi



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na watendaji kutoka Wizara hizo pamoja na TANESCO wakiwa katika mitambo ya umeme ya Kinyerezi II inayozalisha umeme wa megawati 240 mkoani Dar es Saalam.*

huo wa Julius Nyerere ambacho kitakuwa na transoma Sita ambapo transfoma Nne zitapoza umeme kutoka kV 400 kwenda kV 220 na transfoma nyingine Mbili zitapoza umeme hadi kV 132 .

Alieleza kuwa mpaka sasa wameyatambua maeneo ya kulipa fidia wananchi waliopisha maeneo yao kupisha ujenzi wa kituo hicho na kwa sasa wanakamilisha taratibu za mwisho kabla ya kuanza kulipa fidia.

Wakiwa mkoani Dar es Salaam Viongozi hao walikagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme katika eneo la Kinyerezi ambapo Mhandisi mradi kutoka TANESCO, Deogratius Nyamtumbega alisema kuwa, kituo hicho kitakuwa na msongo wa kilovoti 400.

Alieleza kuwa, katika kituo cha Kinyerezi kutakuwa na transfoma nne za 250 MVA ambazo zitapoza umeme kutoka kV 400 kwenda kV 220 ambapo kituo hicho kitasambaza umeme katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na mahitaji.

Baada ya ukaguzi wa maeneo hayo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru alishukuru Wizara ya Nishati na TANESCO kwa kuwaonyesha viongozi hao kutoka Wizara ya Fedha kile kinachotekelezwa na Serikali kwa sasa ili waone maendeleo yake.

Aidha, alitoa wito kwa Taasisi hizo kufanya kazi kwa pamoja ili mradi huo wa kimkakati usikwame.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alieleza kuwa, Wizara ya Nishati na TANESCO zimefarijika kwa viongozi hao wa Wizara ya Fedha kutembelea mradi wa umeme wa Julius Nyerere kwani hiyo ni mdau muhimu katika utekelezaji wa mradi huo.

Alitoa wito kwa viongozi wa Wizara hiyo kutembelea miradi mingine ya kimkakati inayosimamiwa na Wizara ya Nishati.

Viongozi hao kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Nishati, walitembelea pia mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi II ambao unazalisha umeme wa kiasi cha megawati 240.



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali pamoja na watendaji kutoka Wizara hizo pamoja na TANESCO wakiwa katika chumba cha kuendeshea mitambo ya umeme ya Kinyerezi II inayozalisha umeme wa megawati 240 mkoani Dar es Saalam.*

# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 24.7 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 53 KATAVI



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akizungumza na wanakijiji wa Katambike (Hawamo pichani) tarehe 12 Julai, 2021, alipotembelea kijiji hicho kilichopo katika Kata ya Ugalla, wilaya ya Mpanda, Halmashauri ya Nsimbo, Mkoa wa Katavi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo.*

**Na Dorina Makaya - Katavi**

Serikali itatumia zaidi ya shilingi bilioni 24.7 kuunganisha umeme kwenye vijiji 53 ambavyo bado havijaunganishiwa umeme mkoani Katavi katika Mradi Kabambe wa kupeleka umeme vijijini Awamu ya III Mzunguko wa pili.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato tarehe 12 Julai, 2021, alipotembelea kijiji cha Katambike, Kata ya Ugalla, wilaya ya Mpanda, Halmashauri ya Nsimbo, Mkoa wa Katavi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo.

Alisema, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa umeme wa uhakika mkoani Katavi na kuwa MW 5.3 zinazozalishwa katika kituo cha Mpanda bado hazitoshelezi mahitaji ya umeme hususan katika kuwezesha shughuli za kiuchumi na maendeleo ya viwanda na biashara hapa nchini.

Naibu Waziri Byabato alieleza kuwa, Serikali imeamua kupeleka gridi ya Taifa mkoani Katavi ili kuwa na umeme wa uhakika mkoani humo na tayari ujenzi wa majengo ya vituo vya umeme kupeleka gridi ya Taifa mkoani Katavi umefikia zaidi ya asilimia 90.

Alivitaja vituo hivyo kuwa ni Ipole, Inyonga na Mpanda.

Aliongeza kuwa, pesa kwa ajili ya kupeleka umeme mkoani Katavi ipo, na zitawekwa transfoma mbili zenye ukubwa wa 15MVA kila moja sawa na 12MW, zitakazowekwa kwenye kituo cha Inyonga na nyingine katika kituo cha Ipole ili kuhakikisha kila kituo kinatoa umeme wa kutosha na wa uhakika.

Naibu Waziri Byabato alisema, mradi wa Gridi ya Taifa kwa mkoa wa Katavi utakamilika ifikapo Agosti, 2023.

Aliwaeleza wananchi wa kijiji cha Katambike kuwa, umeme utakuwa umefika kijijini hapo ifikapo mwezi Octoba mwaka 2021, na kuwa hakuna kijiji kitakachoachwa kuunganishiwa umeme.

Aliwaasa wanakijiji cha Katambike kuanza kufanya maandalizi

# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 24.7 KUVIPELEKEA UMEME VIJIJI 53 KATAVI

ya kupokea umeme kwa kuanza kutandaza nyaya kwenye nyumba zao (Wiring) na kulipia shilingi elfu 27,000 tu ili waweze kuunganishiwa umeme utakapofika kijijini hapo.

Akizungumza wakati wa mkutano huo Mbunge wa jimbo la Nsimbo, Mhe. Anna Lupembe alimshukuru Naibu Waziri Byabato kwa kufika mkoani Katavi, kujionea hali halisi ya umeme mkoani humo na kutoa ahadi ya kuvipelekea umeme vijiji 53 ambavyo bado havijaunganishwa umeme na kuahidi kufikisha umeme kijijini Katambike ifikapo mwezi Octoba 2021.

Mhe. Lupembe, alisema, kupatikana kwa umeme katika kata ya Ugalla kutasaidia sana katika kuinua kilimo cha mpunga na kuwezesha mazingira ya uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vitakavyoboresha bidhaa ya mchele katika viwango vya juu zaidi na kuwaongezea kipato wananchi wa Ugalla.

Awali Naibu Waziri Byabato alitembelea vituo vipya vinavyojengwa vya Ipole, Inyonga na Mpanda na kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa vituo hivyo.

Mara baada ya kuwasili katika wilaya ya Mlele tarehe 11 Julai, 2021 Naibu Waziri Byabato alikutana na Mkuu wa Wilaya ya Mlele Filiberto Sanga na kupata taarifa kuhusu upatikanaji wa umeme Wilayani Mlele.

Aidha tarehe 12 Julai, 2021 kabla ya kuanza ziara yake katika kata ya Ugalla mkoani Katavi, Naibu Waziri Byabato alikutana na Mkuu wa mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Hoza Mrindoko na kupata taarifa ya upatikanaji wa umeme kwa mkoa wa Katavi.



*Wanakijiji cha kijiji Katambike, Kata ya Ugalla, wilaya ya Mpanda, Halmashauri ya Nsimbo, Mkoa wa Katavi wakimsikiliza Naibu Waziri Byabato (Hayumo pichani) alipokuwa akizungumza nao kufuatia ziara yake ya kikazi kijijini hapo tarehe 12 Julai, 2021.*

# BILIONI 18 KUKAMILISHA UPELEKAJI UMEME VIJIJI VILIVYOSALIA KONDOA

**Veronica Simba na Hafsa Omar**

Serikali imetenga kiasi cha takribani shilingi bilioni 18.6 kwa ajili ya kuvifikishia umeme vijiji vyote 42 vilivyopo wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, ambavyo bado havijafikiwa na huduma hiyo.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani wakati akizindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili Ngazi ya Mkoa, uliofanyika Julai Mosi mwaka huu katika Kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa.

"Kijiji cha Itaswi ni moja kati ya vijiji 42 vilivyopo katika Wilaya ya Kondoa ambavyo hadi sasa bado havijafikiwa na huduma ya umeme. Hivyo basi, Serikali kwa kutambua hilo imetenga kiasi hicho cha fedha ili kukamilisha kazi hiyo," alieleza Waziri.

Aidha, katika hafla hiyo, Dkt. Kalemani



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (katikati)

aliwatambulisha Wakandarasi watakaotekeleza Mradi husika wilayani humo, ambao ni kutoka Kampuni ya Ok Electrical and Electronics Service Ltd na kuwataka wananchi ambao hawajafikiwa na umeme kutokuwa na shaka kwani Serikali imejipanga vema kuhakikisha wote wanafikiwa na nishati hiyo.

"Mkoa wa Dodoma kwa ujumla wake una vijiji 387 vyenye umeme kati ya 565 vilivyopo. Leo ninawakabidhi wakandarasi hawa kwenu wananchi ili kwa pamoja waushambulie Mkoa



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021.

# BILIONI 18 KUKAMILISHA UPELEKAJI UMEME VIJIJI VILIVYOSALIA KONDOA



*Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Wakili Julius Kalolo akipunga mikono kuwasalimu wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani).*



*Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga (kulia) akizungumza na wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto).*

huu na kuhakikisha vijiji vyote 178 vilivyosalia vinapatiwa umeme," alisisitiza.

Waziri aliwahamasisha wananchi kukamilisha utandazaji wa nyaya katika nyumba zao mapema ili Mkandarasi atakapofika katika maeneo yao, wawe tayari kulipia na kuunganishiwa umeme.

Aliwashauri wananchi wenye nyumba ambazo siyo kubwa, kutumia kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) ambacho hakihitaji kutandaza nyaya katika nyumba.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini (Rural Energy Board – REB), Wakili Julius Kalolo, alieleza kuwa malengo ya Serikali ni kusambaza nishati ya umeme katika vijiji vyote ifikapo Disemba 2022 na vitongoji vyote mwaka 2025.

Wakili Kalolo alieleza zaidi kuwa, utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, utaongeza uwekezaji wa miradi katika sekta mbalimbali vijijini ikiwa ni pamoja na kuanzishwa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

"Aidha, miradi hii itaongeza ufanisi katika sekta ya madini kwa kufikisha umeme katika migodi ya wachimbaji wa madini hususani wachimbaji wadogo na wa kati," alieleza Mwenyekiti.




*Mbunge wa Kondoa, Dkt. Ashatu Kijaji akizungumza na wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani).*

# BILIONI 18 KUKAMILISHA UPELEKAJI UMEME VIJIJI VILIVYOSALIA KONDOA

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga alieleza kuwa kuanzishwa kwa Wakala huo na utashi wa dhati wa Serikali, kumeleta mageuzi makubwa ya Sekta ya Nishati Vijijini ambapo upatikanaji wa umeme umeongezeka kutoka vijiji 518 sawa na asilimia 4 ya vijiji 12,268 mwaka 2007 hadi kufikia vijiji 10,312 sawa na asilimia 84 mwezi Machi, 2021.

Mhandisi Maganga alibainisha kuwa mafanikio hayo yamepatikana kufuatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini (REF) kuanzia mwaka 2008, ambapo kiasi cha zaidi ya shilingi trilioni 3.5 zimewekezwa. Uwekezaji huo umewezesha utekelezaji wa miradi kufikia hatua ya vitongoji.

“Hadi sasa, umeme umefika katika Wilaya zote. Aidha, Kata 3,225 kati ya 3,956 sawa na asilimia 82 na Vitongoji 26,860 kati ya 64,384,” alibainisha.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya viongozi wilayani humo akiwemo Mkuu wa Wilaya, Hamis Mkananchi na Mbunge



*Wajumbe wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Oswald Urassa (kushoto) na Louis Accaro (kulia), wakifuatilia matukio mbalimbali wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani), kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma,*



*Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Hamis Mkananchi akizungumza na wananchi wa kijiji cha Itaswi, wilayani Kondoa, Mkoa wa Dodoma, wakati wa hafla ya kuzindua Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Ngazi ya Mkoa, Julai 1, 2021. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani).*

wa Jimbo la Kondoa, Dkt. Ashatu Kijaji walipongeza kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Serikali katika kupeleka umeme vijijini, hususani katika Wilaya hiyo.

Hata hivyo, viongozi hao waliomba kazi ya kukamilisha upelekaji umeme katika vijiji vilivyosalia, itekelezwe kwa kasi ili kukidhi kiu ya wananchi ambao wamejiandaa kupokea nishati hiyo ili waitumie katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo hivyo kuboresha maisha yao.

Hafla hiyo ya uzinduzi ilihudhuriwa pia na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali, Wajumbe wa Bodi ya Nishati Vijijini Mhandisi Francis Songela, Louis Accaro, Oswald Urasa na viongozi wengine mbalimbali pamoja na wananchi.

# TUMIENI FURSA YA UMEME KWA SHUGHULI ZA MAENDELEO - NAIBU WAZIRI BYABATO



**Na Dorina G. Makaya - Simiyu**

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Wakili Stephen Byabato amefanya uzinduzi wa Mradi wa kusambaza umeme vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili kimkoa mkoani Simiyu katika kijiji cha Igwata kata ya Nyabubinza wilayani Maswa .

Naibu Waziri Byabato alisema tarehe 08/07/2021 kuwa, jumla ya vijiji 151 kwa mkoa mzima vitapatiwa huduma ya umeme ambapo Wilaya ya Maswa ni vijiji 13, Bariadi 35, Meatu 48 na Busega vijiji 4 pamoja na vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na huduma ya umeme pia vitafikiwa vyote bila kubakiza hata kimoja.

Naibu Waziri Byabato aliwataka wananchi kushirikiana na Serikali ili kutoa ardhi na maeneo yao ili miundombinu ya umeme ipite ili waweze kupata huduma ya umeme na kuboresha maisha yao na huduma za kijamii.

Alisisitiza kuwa, bei ya umeme ni shilingi 27,000 kwa wateja wanaohitaji njia moja ya kusafirishia umeme (single phase) na 139,000 kwa wateja wanaohitaji njia tatu za kusafirishia umeme (Three phase).

Aliwasisitiza wananchi kuchangamkia fursa hiyo ya kuunganishiwa umeme ambayo ni kichocheo muhimu cha maendeleo.

Aidha, Mhe. Byabato alimuagiza Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili kuwasha umeme katika kijiji cha Igwata ndani ya mwezi mmoja kuanzia leo tarehe 08/07/2021.

Kwa upande wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Naibu Waziri wa Nishati, aliagiza kufunguliwa kwa madawati ya kutolea huduma ili kuwasaidia wananchi kutopata usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kulipia huduma ya umeme.

Aliwasisitiza wananchi kushirikiana na TANESCO ili kuwaongoza kupata wakandarasi wanaofunga umeme majumbani ili kukwepa kutapeliwa na vishoka.

Naibu Waziri Byabato aliwashauri wananchi ambao bado hawapo tayari kuweka mtandao wa nyaya katika nyumba zao kutumia kifaa cha UMETA (Umeme tayari) ambacho mwananchi atafungiwa kwa 27,000 tu.



# GRIDI YA TAIFA KUUNGANISHWA KATIKA KISIWA CHA MAISOME

**Hafsa Omar- Mwanza**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka umeme wa gridi ya Taifa katika kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza.

Agizo hilo amelitoa, Julai 18, 2021 wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi umeme wa jua unaotekelezwa katika kisiwa hicho.

Akizungumza na wananchi, alisema kuwa suluhisho la kudumu la kutatua tatizo la umeme katika kisiwa hicho ni kuunganishwa na gridi ya Taifa.

"TANESCO na REA nataka mkajipange ndani ya miezi mitatu mlete umeme wa gridi huku, Serikali inawaletea umeme wa kudumu wa gridi ya Taifa ambao utasaidia kuondoa hizi changamoto zote,"alisema

Aidha, alisema Serikali itahakikisha kuwa Watanzania wote wanapata umeme wa uhakika na wa bei nafuu kwa wakati wote.



*Wananchi wa kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi umeme wa jua unaotekelezwa katika kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza, Julai 18, 2021.*

Alisema, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 5.2 kwa ajili ya kupeleka umeme wa jua (Solar) kwenye eneo hilo ili wananchi wapate huduma hiyo.

Dkt. Kalemani alitoa agizo kwa kampuni inayosambaza umeme katika kisiwa hicho ya JUMEME kuwauzia umeme wananchi kwa bei ya uniti moja kwa shilingi 100 ili wananchi hao wapate umeme wa bei nafuu.

"Walikuwa wanauza umeme kwa shilingi 3700 kisha 3500 wakaja na 2500 lakini kuanzia Alhamisi bei ya umeme



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani( kwanza-kushoto) akizungumza na wananchi wa kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza, wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi umeme wa jua unaotekelezwa katika kisiwa hicho, Julai 18, 2021.*

# GRIDI YA TAIFA KUUNGANISHWA KATIKA KISIWA CHA MAISOME



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanoni, wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi umeme wa jua unaotekelezwa katika kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza, Julai 18, 2021.*



*Miundombini inayotumiwa kuzalisha umeme wa jua na Kampuni ya JUMEME iliyopo katika kisiwa cha Maisome, kilichopo Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza, Julai 18, 2021.*

huku siku zote itakuwa ni shilingi 100 kwa uniti basi, Mhe Rais anataka watanzania wote wapate umeme tena umeme wa bei nafuu," alisema

Alifafanua kuwa, Serikali mwaka juzi iliwaita wazalishaji wote wa umeme nchini na kuwaelekeza kuuza umeme kwa bei elekezi ambayo haitawaumiza Watanzania.

Pia, aliwataka wasambazaji hao kutoa huduma hiyo kwa masaa 24 bila ya kuwawekea mgao au kukatika bila ya sababu maalum, kwakuwa wananchi hao wanahitaji huduma hiyo kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Vilevile, aliwaagiza wasambazaji hao kufungua ofisi katika eneo hilo ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi na kwa wakati wote na kuwataka kuendelea kusambaza umeme kwenye vitongoji vyote vilivyobaki.

Naye, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Erick Shigongo, alimshukuru Waziri wa Nishati, kwa kazi nzuri anayofanya ya usimamizi wa usambazaji wa umeme na kwa kutatua mzozo wa bei ya umeme katika kisiwa hicho.

Pia, aliwataka wananchi wa kisiwa hicho kuendelea kutumia huduma hiyo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

# VIJIJI 192 VILIVYOBAKI MKOA WA LINDI KUFIKIWA NA UMEME



Naibu Waziri wa Nishati akiwa ameshikilia utepe kwa ajili ya kuukata na kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili mkoa wa Lindi tarehe 03 Julai, 2021.

**Na Dorina G. Makaya - Lindi**

Naibu Waziri wa Nishari Mhe. Wakili Stephen Byabato amesema, jumla ya vijiji 192 kati ya vijiji 524 vilivyopo mkoani Lindi, vinakwenda kupatiwa huduma ya umeme,baada ya kuzinduliwa kwa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika mkoa wa Lindi.

Aliyasema hayo tarehe 03 Julai, 2021 alipokuwa akifanya uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika kijiji cha Narungombe, Wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayo azma madhubuti kabisa ya kuhakikisha watanzania wote wanapata umeme kwa ajili ya kufanya shughuli za kijamii pamoja na za kiuchumi na kuwa



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Wakili Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa kijiji cha Narungombe (hawapo pichani) wilayani Ruangwa, mkoani Lindi alipokwenda kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili tarehe 03 Julai, 2021.

# VIJIJI 192 VILIVYOBAKI MKOA WA LINDI KUFIKIWA NA UMEME

umeme huo unaletwa na Serikali kwa asilimia mia moja.

Aliwataka wakandarasi kutekeleza mradi huo kwa wakati ili wananchi waweze kunufaika na miradi ambayo serikali inatekeleza kwa ajili yao.

Aliwataka wananchi kutumia fursa hiyo ya kujiunganishia umeme utakapokuwa tayari na kuwa kwa sasa waanze kutandaza nyaya kwenye nyumba zao ili kujiandaa na fursa iliyojitokeza ya kuunganishiwa umeme.

Aidha aliwataka wananchi kuitunza miundombinu ya umeme ili idumu kwa kuacha tabia ya kuchoma moto maeneo yenye nguzo za umeme kwani Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa katika kuweka miundombinu ya umeme kwenye maeneo yao kwa lengo la kuwanufaisha wananchi.

Naibu Waziri Byabato, aliwataka watumishi wa TANESCO kuwachukulia hatua wale watakaobainika kuhujumu miundombinu hiyo ya umeme.

Aidha Mh. Byabato, alimuagiza Meneja wa TANESCO mkoa wa Lindi Mha. Kainda Museru Kuhakikisha anahamishia ofisi ya malipo vijijini ili kuwarahisishia na kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kwenda katika ofisi za makao makuu ya mkoa ama wilaya kufanya huduma za malipo.



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Wakili Stephen Byabato akimkabidhi mama Opeta Sijui Bure kifaa cha UMETA (Umeme Tayari) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwake katika Kijiji cha Narungimbe, wilayani Ruangwa, Mkoa wa Lindi alipokwenda kuzindua Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili tarehe 03 Julai, 2021*

# WAZIRI KALEMANI AZINDUA MRADI WA PERI URBAN

**Hafsa Omar na Veronica Simba- Mwanza**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, amezindua Mradi wa Kusambaza Umeme awamu ya pili katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza (Peri Urban).

Tukio hilo lilifanyika katika mtaa wa Igogwe, kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza.

Akizungumza na wananchi, alisema kuwa Serikali imetoa zaidi ya shilingi Bilioni 9 kuhakikisha kuwa inakwenda kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma ya umeme katika maeneo ya pembezoni mwa jiji hilo.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa mtaa wa Igogwe, kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza (hawapo pichani) wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme awamu ya pili katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza (Peri Urban), Julai 9,2021.*

Alifafanua kuwa, maeneo hayo wamechelewa kupata umeme kwakuwa hayakuwa na sifa ya kupata umeme wa 27,000 lakini kwasababu Serikali ni sikivu imeamua maeneo yote ya mjini yanayofanana na kijijini yapelekewe umeme kwa 27,000.

" Tulipoanza kusambaza umeme vijijini tukajikuta tumepeleka umeme mwingi vijijini maeneo mengi ya mijini tena yana sura sawa na vijijini hayakuwa na umeme lakini kwasasa kutokana na mradi huu maeneo yote kama haya yatapata umeme wa bei nafuu,"alisema.

Aidha, alimtaka mkandarasi kuhakikisha anasambaza umeme katika maeneo yote ya mitaa hiyo ndani ya miezi 12 ili wananchi wa maeneo hayo waanze mara moja kupata huduma hiyo muhimu.

Aliongeza kuwa, kwakuwa eneo hilo nyumba zipo karibu,hivyo itakuwa rahisi kwa mkandarasi kukamilisha kazi hiyo kwa haraka na kuwataka wananchi



*Mbunge wa jimbo la Ilemela, Angeline Mabula akizungumza na wananchi wa mtaa wa Igogwe, kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza (hawapo pichani) wakati wa uzinduzi wa amezindua wa Mradi wa Kusambaza Umeme awamu ya pili katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza (Peri Urban), Julai 9,2021.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akikata utepe kuashiria kwa kuwasha kwa umeme katika zahanati Nyamwilolelwa iliyopo katika mtaa wa Nyamwilolelwa, Kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza, Julai 9,2021.*

# WAZIRI KALEMANI AZINDUA MRADI WA PERI URBAN

kutoa ushirikiano kwa mkandarasi huyo ili kazi ikamilike mapema.

Alisema kuwa, Taasisi za umma zipewe kipaumbele kuunganishiwa umeme kwakuwa maeneo hayo ni muhimu katika jamii na bila huduma hiyo hawataweza kutoa huduma bora.

Alisisitiza kuwa, wananchi wakikamilisha malipo ya kupata huduma ya umeme waunganishiwe na huduma hiyo ndani ya siku 14 ili wananchi hao waanze kutumia umeme kwa kujiletea maendeleo mbalimbali.

Vilevile, alimtaka mkandarasi kutumia nguzo za zege kusambazia umeme kwakuwa zinadumu kwa muda mrefu na zitaondoa tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa tatizo la kuanguka kwa nguzo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angeline Mabula, aliishukuru Serikali kwa uamuzi wa kuleta mradi wa Peri Urban, kwani umekuwa mkombozi kwa wananchi wa jimbo hilo na kuwataka wananchi kutumia fursa hiyo kwa kuunganisha umeme huo majumbani na kutumia kwa shughuli za kiuchumi.

Naye, Meneja Miradi ya Umeme Vijiji, Kanda ya Ziwa, Mhandisi Ernest Makale, alisema mradi huo mkubwa unatarajia kuunganisha umeme wananchi zaidi ya 10224.

Alieleza kuwa, uhitaji wa umeme ni mkubwa lakini Serikali imejipanga na itahakikisha kila mwananchi anafikiwa na huduma hiyo.

Dkt. Kalemani, pia aliwasha umeme katika zahanati ya Nyamwilolelwa iliyopo katika mtaa wa Nyamwilolelwa, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza.



*Meneja Miradi ya Umeme Vijiji, Kanda ya Ziwa, Mhandisi Ernest Makale, akizungumza na wananchi wa mtaa wa Igogwe, kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza (hawapo pichani) wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme awamu ya pili katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza (Peri Urban), Julai 9,2021.*



*Wananchi wa mtaa wa Nyamwilolelwa, Kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(katikati) kabla ya kuwasha umeme kwenye zahanati ya mtaa huo, Julai 9,2021.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akiwatambulisha kwa wananchi wakandarasi, Kampuni Namis Corporate Ltd wanaotekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme awamu ya pili katika maeneo ya pembezoni mwa jiji la Mwanza (Peri Urban). Waziri alizundua mradi katika mtaa wa Igogwe, kata ya Chibula, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza, Julai 9,2021.*

# Wizara ya Fedha yaridhishwa na maboresho ya Kituo cha umeme Zuzu

**Na Teresia Mhagama, Dodoma**

Wizara ya Fedha na Mipango imeeleza kuridhishwa kwake na maboresho yanayoendelea kufanyika katika Kituo cha Umeme cha Zuzu mkoani Dodoma ambacho kimeongezewa uwezo kutoka megawati 48 hadi megawati 648.

Hayo yalibainishwa tarehe 26 Julai, 2021 wakati wa ziara Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Fedha na Mipango walioongozwa na Kamishna wa Fedha za Nje, Sauda Msemo ambaye alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo.

Kituo hicho, ambacho awali kilikuwa na uwezo wa megawati 48 kwa sasa kimeongezewa transfoma ambazo kwa ujumla zinafanya kituo hicho kuwa na uwezo wa megawati 648 na hivyo kupelekea umeme mkoani Dodoma kuwa wa uhakika na kuongezeka kwa laini zinazopeleka umeme katika maeneo mbalimbali.



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Kamishna wa Fedha za Nje, Sauda Msemo (wa kwanza kushoto) wakikagua kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Wengine katika picha ni viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO*

"Tumekuja kuangalia kituo hiki cha Zuzu ili kuona hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, na kuelewa kazi zilizobaki ili kukamilisha mradi na kama kuna changamoto zinazohitaji kutatuliwa ili kuweza kukamilisha mradi ili kupata matokeo yaliyotarajiwa." Amesema Msemo

Alisema kuwa, Wizara hiyo imeridhishwa na hatua iliyofikiwa hadi sasa na pia mikakati iliyowekwa ili kukamilisha mradi huo na kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Nishati katika utekelezaji wa miradi mbalimbali na imekuwa ikitoa fedha kwa wakati



*Transfoma mbili zilizofungwa katika kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma ambazo zimeongeza uwezo wa umeme wa Kituo hicho.*

# Wizara ya Fedha yaridhishwa na maboresho ya Kituo cha umeme Zuzu

kutekeleza miradi ya Nishati.

Aliongeza kuwa, katika ziara hiyo wamepata uelewa wa masuala mbalimbali ikiwemo umuhimu wa uwepo wa vituo vya uzalishaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kuwa na uhakika wa uwepo wa umeme na usalama wake.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alisema kuwa, ziara hiyo imekamilisha ziara ya viongozi hao katika miradi mbalimbali ya Nishati iliyoanzia katika mradi wa umeme wa Julius Nyerere, na kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ni wadau muhimu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Nishati hivyo ziara hiyo imesadia kupata uelewa wa pamoja utakaorahisisha majadiliano na maamuzi



*Mratibu wa Mradi kutoka TANESCO, Mhandisi Peter Kigadye akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa Tano, kulia) na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Kamishna wa Fedha za Nje, Sauda Msemo ( wa Sita kulia) wakati wakikagua kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Wengine katika picha ni viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO*

yanayofanyika.

Alitoa wito kwa wadau wengine kutembelea miradi ya nishati ili kujenga uelewa wa pamoja utakaosaidia kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwani nishati ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi, Mhandisi Peter Kigadye alisema kuwa upanuzi wa kituo umehusisha kuongeza uwezo kituo kwenda kV 220 na sasa kinaongezewa uwezo wa kV 400 ambao kwa ujumla kufanya kituo hicho kuwa na uwezo wa megawati takriban 648.

Aliongeza kuwa, kituo hicho pia kitapokea umeme kutoka mradi wa umeme wa Julius Nyerere na kupeleka maeneo ya mbalimbali ya nchi. Mradi wa upanuzi wa Kituo cha Zuzu unatarajiwa kukamilika rasmi mwezi Septemba mwaka huu.



*Mratibu wa Mradi kutoka TANESCO, Mhandisi Peter Kigadye akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Kamishna wa Fedha za Nje, Sauda Msemo wakati wakikagua kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Wengine katika picha ni viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO*

# Fedha za Watanzania zinatumika ipasavyo JNHPP- Wizara ya Fedha

**Na Teresia Mhagama, Pwani**

Wizara ya Fedha na Mipango imeeleza kuwa, fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) wa megawati 2115 zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Hayo yalisemwa tarehe 20 Julai, 2021 na Kamishna wa Fedha za Nje wa Wizara ya Fedha na Mipango, Sauda Msemo ambaye alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo katika ziara ya viongozi mbalimbali wa Wizara husika katika mradi huo.



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiwa katika picha ya pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali wakati walipotembelea mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere mkoani Pwani. Wa Nne kutoka kulia ni Kamishna wa Fedha za Nje kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Sauda Msemo na wa Tano kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka*

Ziara hiyo iliongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali ambaye aliambatana na viongozi mbalimbali wa Idara na Vitengo kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Msemo alisema kuwa ziara ya viongozi hao wa Wizara ya Fedha na Mipango imefanyika kwa madhumuni kuona kama fedha zinazoingizwa kwenye mradi zinatumika kama ambavyo mipango ya Serikali inavyoelekeza.

"Tumetembelea maeneo mbalimbali na kwa kweli tumeridhishwa na hatua iliyofikiwa, maendeleo ni mazuri na tumeona jitihada za Serikali katika kusimamia mradi huo na kuhakikisha umetekelezwa ndani ya muda uliopangwa." Alisema Msemo

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, alisema kuwa, Makamishna na Wakurugenzi hao wa Wizara ya Fedha na Mipango, walitembezwa katika maeneo



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati wakiwa katika kikao na viongozi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (hawapo pichani) kabla ya kukagua mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere unaotekelezwa mkoani Pwani. Wa kwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.*

# Fedha za Watanzania zinatumika ipasavyo JNHPP- Wizara ya Fedha



*Sehemu ya ujenzi wa mradi wa umeme wa maji Julius Nyerere ukiendelea ambapo baada ya kukamilika utazalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.*

mbalimbali ya utekelezaji wa mradi ikiwemo jengo la mitambo ya kuzalisha umeme, handaki la kupeleka maji kwenye mitambo, kingo za kuzuia maji yasitoroke katika bwawa na kituo cha kupokea na kusafirisha umeme.

Aliongeza kuwa, Wizara ya Nishati ambayo ni msimamizi wa mradi huo imefarijika baada ya kuona kuwa viongozi hao wameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi kwani Wizara ya Fedha ndiyo inayotoa fedha hizo kwa niaba ya Serikali.

Aliongeza kuwa, makundi mbalimbali yamekuwa yakitembelea mradi huo ikiwemo wananchi na viongozi kwani mradi huo ni wa kimkakati na hivyo wanahitaji kuona uhalisia wake kwani mradi huo una umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa JNHPP, Mhandisi Mkazi wa Mradi, John Mageni alisema kuwa, ujenzi wa maeneo muhimu matano ambayo yanahusika moja kwa moja na uzalishaji umeme umefikia asilimia 54.3

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni, ujenzi wa tuta kuu, jengo la mitambo ya kuzalisha umeme, handaki la kupeleka maji kwenye mitambo, kingo za kuzuia maji yasitoroke katika bwawa na kituo cha kupokea na kusafirisha umeme.

Kuhusu ajira, alieleza kuwa, mpaka kufikia mwezi Juni, 2021, jumla ya watanzania 6,650 wameajiriwa katika mradi huo wa JNHPP.



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Nishati, wakiangalia kazi za ujenzi wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere wakati walipotembelea mradi huo.*



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiwa katika kikao na viongozi kutoka Wizara ya Nishati (hawapo pichani) kabla ya kukagua mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere unaotekelezwa mkoani Pwani. Wa kwanza kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali. Wa kwanza kutoka kushoto ni Kamishna wa Fedha za Nje kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Sauda Msemo*

# WANANCHI WAPATA ELIMU YA SEKTA YA NISHATI SABASABA

Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara, wamefanikiwa kutoa elimu ipasavyo kwa wananchi kuhusu Sekta ya Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.




*Wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati wakiwa katika picha ya Pamoja kabla ya kuanza kutoa elimu kwa wananchi katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*

Katika Maonesho hayo wananchi walielezwa kuhusu masuala mbalimbali kama utekelezaji miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na Gesi Asilia.

Aidha, Wataalam hao walipokea maoni




*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati (kutoka kulia), Arnold Shada, Jacob Mayalla na Mwanamani Kidaya wakimsikiliza mwananchi aliyefika katika Banda la Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*



*Mtaalam kutoka Wizara ya Nishati, Shukrani Rugaimukamu akitoa elimu mwananchi aliyefika katika Banda la Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*

# WANANCHI WAPATA ELIMU YA SEKTA YA NISHATI SABASABA

na kutoa huduma mbalimbali ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazoshiriki Maonesho hayo.

Taasisi zilizo chini ya Wizara zilizoshiriki Maonesho hayo ni pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Kauli Mbiu ya Maonesho hayo ilikuwa, Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu ambapo nishati ni injini ya kuwezesha uchumi huo wa viwanda.

Katika Maonesho hayo, Wizara ya Nishati ilifanikiwa kuibuka mshindi wa Tatu katika kundi la Wizara, Taasisi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.



*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati (kutoka kulia), Jacob Mayalla, Shukrani Rugaimukamu na Mussa Abbas wakimsikiliza mwananchi aliyefika katika Banda la Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*



*Mtaalam kutoka Wizara ya Nishati, Jacob Mayalla (katikati) akitoa elimu kwa wananchi kuhusu Sekta ya Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*



*Mtaalam kutoka Wizara ya Nishati, Mussa Abbas akitoa elimu kwa wananchi kuhusu Sekta ya Nishati katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.*

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*